EdTech Hub

Ubainisho wa wazi, maamuzi mazuri, ujifunzaji zaidi

# Usawa na Maamuzi katika Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini yanayowezeshwa na Teknolojia nchini Tanzania

Zana za utafiti

**Tarehe** Julai 2025

**Waandishi** Timu ya Utafiti wa MEWAKA nchini Tanzania iliyoongozwa na EdTech Hub

**DOI** 10.53832/edtechhub.1097

@GlobalEdTechHub edtechhub.org

Creative Commons Attribution 4.0 International https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

# Kuhusu ukurasa huu

**Nukuu inayopendekezwa**

Chachage, K., Swai, C., Rwambali, I., Hennessy, S., Koomar, S., Massam, W., Jacob, W., Gervace, A., Malibiche, M., Mutura, E., Adam, T., Mwakabungu, F., Mrosso, V., Komba, P. & Mtenzi, F. (2025). *Usawa na maamuzi katika Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini yanayowezeshwa na Teknolojia nchini Tanzania: Zana za utafiti*. EdTech Hub. https://doi.org/10.53832/edtechhub.1097. Inapatikana katika https://docs.edtechhub.org/lib/IQXW2UG5. Inapatikana chini ya Creative Commons Attribution 4.0 International, https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/.

**Leseni**

Creative Commons Attribution 4.0 International
https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

Kwenu — wasomaji wapendwa — mko huru kunakili na kusambaza zana hizi za utafiti katika hali au muundo wowote na kuzichanganya, kubadilisha, na hata kuboresha kwa madhumuni yoyote, hata kibiashara. Hata hivyo ni lazima utambue kwa usahihi waliotengeneza zana hii, utoe linki ya kimtandao kuelekea leseni ilipo, na uonyeshe ikiwa mabadiliko yalifanywa. Unaweza kufanya hivyo kwa njia yoyote inayofaa, lakini si kwa njia yoyote inayoonesha mtoa leseni anakufahamu au anafahamu namna utakavyotumia zana hizi.

# Kuhusu EdTech Hub

EdTech Hub ni ushirika wa kimataifa wa utafiti usio wa faida. Lengo letu ni kuwahamasisha watu kwa kuwapa ushahidi wanaohitaji kufanya maamuzi kuhusu teknolojia katika elimu. Maktaba yetu ya ushahidi ni hazina ya utafiti wetu wa hivi punde, matokeo na fasihi pana kwenye teknolojia ya elimu. Kama ushirikiano wa kimataifa, tunanuia kufanya ushahidi wetu upatikane na ufikiwe na wale wanaotafuta suluhisho ya teknolojia ya elimu ulimwenguni.

EdTech Hub inafadhiliwa na UKAid, Bill & Melinda Gates Foundation, World Bank, na UNICEF. Maoni katika hati hii sio lazima yaambatane na maoni ya mashirika haya.

Kupata taarifa zaidi kuhusu EdTech Hub, tembele tovuti yetu kwenye edtechhub.org/. Maktaba yetu inapatikana kwenye docs.edtechhub.org/lib/.

# Usawa na maamuzi katika Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) yanayowezeshwa na Teknolojia nchini Tanzania: Zana za Utafiti (Kiswahili)

Sehemu hii ina zana za utafiti zilizotengenezwa na EdTech Hub, Chuo Kikuu cha Dodoma, chuo kikuu cha Aga Khan, na Taasisi ya Elimu Tanzania kwa ajili ya awamu ya pili ya utafiti (2023-25) unaochunguza upanuzi na mabadiliko ya kuendana na mahitaji ya walimu na mazingira ya shule katika utekelezaji wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) unaojumuisha matumizi ya teknolojia. Katika kuandaa zana hizi, tumetumia zana zilizochapishwa katika awamu ya kwanza ya utafiti huu na mifano kutoka sehemu mbalimbali[1]. Kwa maelezo zaidi kuhusu utafiti huu, tafadhali tembelea ukurasa wetu kwenye mtandao[2].

Maswali ya utafiti kwa awamu ya pili ya utafiti huu:

- 1: Je, maudhui ya programu ya MEWAKA, muundo na utaratibu umeundwa kwa namna ili kukidhi na mahitaji mbalimbali? Je, mabadiliko yanashamirishwa katika ngazi mbalimbali za MEWAKA kwa vitendo? (Kielelezo 1)
  - 1A: Je, ni mbinu gani zipo kiutendaji ili kusaidia kukidhi mahitaji ya walimu wakati wa utekelezaji katika ngazi za kitaifa, wilaya, shule, na JzK (kwa mfano. kupitia chaguzi za moduli au uwezeshaji rika wakati wa JzK)? Je, matarajio kuhusu mabadiliko ya muundo wa MEWAKA yanatimizwa katika kila ngazi?
  - 1B: Je, mabadiliko mapya ya yasiyotarajiwa yanatokea? Je, mabadiliko hurekodiwaje, yanapatiwa mrejesho, na kutekelezwa kupitia muundo uliogatuliwa wa mfumo wa MEWAKA?

[1] Angalia Koomar, S., Massam, W., Jacob, W., Gervace, A., Adam, T., Hennessy, S., Chacage, K., Malibiche, M., Mutura, E., Mtenzi, F., & Mwakabungu, F. (2023). *Teknolojia na maendeleo ya taaluma ya walimu nchini Tanzania: Zana za utafiti* [Research Instruments and Tools / Zana za utafiti]. EdTech Hub. https://doi.org/10.53832/edtechhub.0149. Inapatikana katika https://docs.edtechhub.org/lib/GXM765F3.

[2] Angalia https://edtechhub.org/evidence/edtech-hub-research-portfolio/impact-of-tech-supported-tpd-model-on-learning-tanzania/. Retrieved 5 June 2025.

  - 1C: Je, kuna uwiano ufaao kati ya usanifishaji na utoaji wa maamuzi ya mabadiliko shuleni na viwango vya walimu?

- 2: Je, MEWAKA inasaidia kwa kiasi gani mahitaji mbalimbali na ushiriki sawa wa makundi mbalimbali ya walimu (jinsia, ulemavu, vijijini na upatikanaji wa teknolojia, uzoefu wa kufundisha, kiwango cha elimu/sifa)?

  - 2A: Ni kwa njia gani programu inakidhi mahitaji mbalimbali ya walimu kwa usawa? (kwa mfano je, walimu wote wanafikia MEWAKA na kushiriki ipasavyo katika vipindi vya JzK?)

  - 2B: Je, mabadiliko yoyote yameonekana (yanayohusishwa na kupanua wigo wa MEWAKA) katika ufundishaji na ujifunzaji au katika maarifa na mitazamo ya walimu inayotofautishwa kulingana na kundi la walimu?

  - 2C: Je, ni vipengele gani vya mafanikio na vikwazo katika MEWAKA (Mchoro 3) katika kusaidia walimu wote? (kwa mfano ufikiaji wa matini za MEWAKA, usaidizi endelevu wa wawezeshaji rika au mafunzo yasiyo rasmi kupitia mitandao ya kijamii)?

- RQ3: Je, ni mafanikio na changamoto gani zilizopatikana wakati wa kutekeleza MEWAKA kitaifa (ikiwa ni pamoja na kulinganisha na majaribio madogo yaliyotangulia)?

Tunaweka zana hizi zipatikane kwa watafiti wengine na watendaji tukitumai kuwa zitakuwa za manufaa. Zana hizi zinapatikana kwa fomati inayoweza kuhaririwa ili wengine waweze kuhariri inavyofaa kwao. Kuna baadhi ya marejeleo ya shughuli zetu za mradi ambayo yanaweza kuwa siyo ya muhimu kwa wengine.

Tuko tayari kupokea maoni kuhusu zana zozote zilizoorodheshwa hapa.

Kurasa ambazo zinafuata zina viunganishi vya zana hizo.  Bofya kiunganishi kuangalia zana.

Kuangalia violezo vya unukuzi (transcripts) na kumbukumbu za utafiti (research memos) ambavyo vinaendana na zana hizi, tafadhali angalia zana zilizochapishwa kwa lugha ya kiingereza.

# Viunganishi vya zana za utafiti

## Kifurushi cha Fomu za Ridhaa

**Kifurushi hiki kina:**

- Hati ya ridhaa ya mdomo ya mwalimu
- Hati ya idhini ya maandishi ya mwalimu
- Hati ya ridhaa ya mdomo ya mwalimu mkuu
- Hati ya idhini ya maandishi ya mwalimu mkuu
- Hati ya ridhaa ya mdomo ya mzazi/mlezi wa mwanafunzi
- Hati ya idhini ya maandishi ya mzazi/mlezi wa mwanafunzi
- Hati ya ridhaa ya mdomo ya mshiriki wa utafiti
- Hati ya Idhini ya maandishi ya mshiriki wa utafiti
- Fomu ya idhini ya mtu binafsi–Upigaji picha/Urekodishaji video
- Kuondolewa kwa Idhini

## Kiolezo cha Uchunguzi wa Darasani

## Kiolezo cha Uchunguzi wa Jumuiya za Kujifunza (JzK)

## Kifurushi cha Zana za Majadiliano ya Vikundi Lengwa na Usaili - Raundi ya kwanza

**Kifurushi hiki kina miongozo na zana za:**

Mwongozo wa majadiliano ya kikundi lengwa cha walimu kwa raundi ya kwanza

Usaili Wa Wahabarishaji Muhimu Raundi ya kwanza

- Mwongozo wa mahojiano na mwakilishi wa serikali kuu
- Mwongozo wa usaili kwa Afisa Elimu wa Mkoa (REO)
- Mwongozo wa usaili kwa Afisa Uthibiti Ubora wa Wilaya
- Mwongozo wa usaili kwa afisa elimu kata (WEO)
- Mwongozo wa usaili kwa Mratibu wa Kituo Cha Walimu
- Mwongozo wa mahojiano ya mwalimu mkuu
- Mwongozo wa Mahojiano ya Mwezeshaji Rika na Mwalimu wa Taaluma baada ya uchunguzi wa JzK)

## Kifurushi cha Zana za Majadiliano ya Vikundi Lengwa na Usaili — Raundi ya pili

Mwongozo wa majadiliano ya kikundi lengwa cha walimu kwa raundi ya pili

Mahojiano mafupi na walimu wenye ulemavu au magonjwa sugu

Mwongozo wa majadiliano ya kikundi lengwa cha Mwezeshaji Rika, Mwalimu wa Taaluma na Mwalimu Mkuu

Usaili wa Wahabarishaji Muhimu Raundi ya pili

Mwongozo wa mahojiano na mwakilishi wa serikali kuu

Mwongozo wa usaili kwa Afisa Elimu Taaluma wa Mkoa (RAO)

Mwongozo wa usaili kwa Afisa Elimu Maalumu wa Wilaya

Mwongozo wa usaili kwa afisa elimu kata (WEO)

## Kifurushi cha Dodoso (Surveys)

Dodoso la shule kwa mwalimu mkuu

Dodoso la walimu